

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

614

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 3

Alhamisi, 08 Mei 2014 asubuhi

Maelekezo


1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Vikokotozi na simu za mkononi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika schemu hii.

- Chunguza ramani ya kijiji cha Chocho na kisha jibu maswali yanayofuata:

RAMANI YA KONTUA YA KIJIJI CHA CHOCHO



UFUNGUO

Majengo

Mto
 Barabara

Kipimo: 1: 350 000

KAS

- Mwinuko wa eneo lenye alama ya X ni meta ngapi kutoka usawa wa bahari?
- Badili kipimo ulichopewa kuwa cha maneno.

- (c) Taja maumbile ya nchi yanayooneshwa na herufi **M** na **E**.
 (d) Pima urefu wa barabara kutoka miraba fito 300159 hadi 503141 (andika jibu katika kilometra).
 (e) Chora mkato wa nchi kutoka alama **B** hadi alama **C**.
2. Eleza kwa kifupi aina nne za tabia nchi zinazopatikana katika ukanda wa Afrika Mashariki.
3. Chunguza takwimu za hali ya hewa ya kituo B ulizopewa kwenye jedwali na kisha jibu maswali yanayofuata.
- | Mwezi | J | F | M | A | M | J | J | A | S | O | N | D |
|---------------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|----------|
| Mvua (mm) | 248 | 211 | 215 | 102 | 53 | 10 | 07 | 28 | 51 | 114 | 150 | 206 |
| Jotoridi (°c) | 27 | 26 | 26 | 26 | 25 | 24 | 24 | 26 | 28 | 28 | 28 | 27 |
- (a) Kokotoa wastani wa jotoridi kwa mwaka.
 (b) Tafuta mfiko wa jotoridi.
 (c) Tafuta kiasi cha mvua kwa mwaka kinachopatikana katika eneo hilo.
 (d) Kituo B kinawakilisha aina gani ya tabia nchi? Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako.
 (e) Kituo B kiko kizio gani cha dunia? Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako.
4. (a) Eleza kwa kifupi kwa nini Mstari wa Tarehe wa Kimataifa umepindapinda.
 (b) Mji wa Accra 0° ni saa 2:00 usiku wakati mji Y ni saa 7 usiku. Je, mji Y uko katika longitudo ngapi?
5. Eleza kwa kifupi mambo manne yanayoathiri mtawanyiko wa jotoridi katika uso wa dunia.
6. Bainisha namna nne ambavyo waafrika waliathirika kisiasa kutokana na uvamizi wa wakoloni kutoka bara la Ulaya.
7. Bainisha mafanikio angalau manne yaliyofikiwa na nchi za kiafrika baada ya uhuru.
8. Kwa kutoa mifano, eleza kwa kifupi aina kuu tatu za uchumi wa kikoloni zilizoanzishwa wakati wa ukoloni katika bara la Afrika.
9. Bainisha makubaliano manne yaliyofikiwa na mataifa ya Ulaya katika mkutano wa Berlin uliofanyika kuanzia Novemba 1884 hadi Januari 1885.
10. Eleza kwa kifupi malengo manne ya kuundwa kwa Umoja wa Afrika (AU).

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika kila kipengele.

Kipengele I: Jiografia

11. Fafanua mambo matano yanayosababisha mtawanyiko wa shughuli za kiuchumi nchini Tanzania.
12. Kwa kutoa mifano, bainisha mambo matano ambayo husababisha uchafuzi wa mazingira tunayoishi.

Kipengele II: Historia

13. Eleza chimbuko la binadamu hatua kwa hatua kulingana na mtazamo wa wanasayansi.
14. Bainisha mambo matano yaliyotokea ndani ya Bara la Afrika ambayo yalichochea harakati za kudai uhuru mionganini mwa nchi za kiafrika katika nusu ya kwanza ya karne ya ishirini.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika kila kipengele.

Kipengele I: Jiografia

15. Tathmini mambo matano ambayo mwalimu wa somo la Jiografia anatakiwa kuzingatia kabla ya kutumia Ziara kama mbinu mojawapo ya kufundishia.
16. Eleza hatua ambazo mwalimu wa somo la Jiografia anapaswa kuzingatia wakati wa kutumia njia ya 'fikirisha, jozisha, wasilisha' kama njia ya kufundishia.

Kipengele II: Historia

17. Fafanua sababu zinazoifanya njia ya kunakili nukuu za somo kuwa mionganini mwa njia mbaya katika ufundishaji wa somo la Historia.
18. Eleza faida zisizopungua tano za kutumia njia shirikishî katika kufundisha somo la Historia.